# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA KILIMO

## MAMLAKA YA UDHIBITI WA NAFAKA NA MAZAO MCHANGANYIKO

# TANGAZO

# FURSA YA MAFUNZO YA WAVUNAJI WA PARACHICHI

**Tarehe 17 Februari, 2026**

**UTANGULIZI**

Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) inapenda kuwataarifu wadau wote wa zao la parachichi kuwa, itatoa mafunzo maalum kwa wavunaji 300 wa parachichi (avocado harvesters) katika awamu ya kwanza kwa msimu wa 2025/206. Mafunzo hayo yanalenga kuongeza uelewa na ujuzi wa kitaalam kuhusu mbinu bora za uvunaji, utunzaji wa matunda baada ya kuvuna na viwango vya ubora vinavyohitajika kwa soko la ndani na la nje ya nchi.

**VITUO VYA MAFUNZO**

| Na. | Ukanda | Kituo | Tarehe za Mafunzo |
|---|---|---|---|
| 1. | Kanda ya Nyanda za juu Kusini | Halmashauri ya Njombe Mji - Njombe | 2 & 3 Machi, 2026 |
| 2. | Kanda ya Kaskazini | Halmashauri ya Meru - Arusha | 5 & 6 Machi, 2026 |
| 3. | Kanda ya Ziwa | Halmashauri ya Ngara - Bukoba | 9 & 10 Machi, 2026 |

**WALENGWA WA MAFUNZO**

1. Wavunaji wa parachichi waliopo katika maeneo ya uzalishaji;
2. Vijana na wakulima wanaopenda kujifunza na kuingia katika fursa ya ajira ya uvunaji wa parachichi;
3. Vikundi vya wakulima vilivyosajiliwa au Vyama vya Ushirika wa Mazao Mchanganyiko; au
4. Mtu yoyote mwenye nia na utayari wa kujifunza na kupata ujuzi wa kuvuna parachichi.

**UTARATIBU WA KUWASILISHA MAOMBI**

Waombaji wanatakiwa kuwasilisha taarifa zao kwa njia ya mtandao kupitia barua pepe dcds@copra.go.tz au kupitia ofisi za wakurugenzi wa Halmashauri katika maeneo yao. Taarifa hizo zijumuishe yafuatayo:

1. Jina kamili la mwombaji;
2. Namba ya NIDA ya mwombaji;
3. Jina la Kikundi/Chama cha Ushirika pamoja na orodha ya majina ya wanakikundi/wanachama;
4. Makazi/Eneo anakoishi (Kijiji, Kata, Wilaya na Mkoa);
5. Kazi anazofanya zinazohusiana na zao la parachichi (endapo zipo);
6. Mawasiliano kamili (namba ya simu / na barua pepe kama ipo).

**MUHIMU**

1. Mwisho wa kuwasilisha maombi ni **tarehe 25 Februari, 2026.** Watakaopata nafasi watapewa taarifa rasmi kwa njia ya simu.
2. Waombaji wote watajigharamia usafiri na malazi wakati wa mafunzo.

**Imetolewa na:**

**MKURUGENZI MKUU**
**MAMLAKA YA UDHIBITI WA NAFAKA NA MAZAO MCHANGANYIKO**